

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

689

VITENDO VYA KUJIFUNZA SAYANSI

Muda: Saa 3

Ijumaa, 09 Mei 2014 asubuhi

Maclekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama 40 na sehemu B na C zina alama 30 kila moja.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Ukurasa wa 1 kati ya 3

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. (a) Nini maana ya neno ‘usafi’.
(b) Toa sababu mbili za kufanya usafi wa mazingira.
2. (a) Taja madhara mawili yanayotokana na kutozingatia usafi.
(b) Bainisha vifaa viwili vinavyohitajika katika usafi wa mwili.
3. (a) Eleza umuhimu wa kuloweka nguo kabla ya kuzifua.
(b) Orodhesha madhara matatu yanayotokea usipozingatia usafi wa mwili.
4. Sifa nne za nguo safi ni zipi?
5. (a) Bainisha vitu vinne vinavyounda mazingira.
(b) Mazingira yana umuhimu upi kwa binadamu?
6. Ainisha njia nne zinazothibitisha kuwa magonjwa yanaweza kuambukizwa kutoka kwa binadamu mmoja hadi mwingine.
7. (a) Bainisha shughuli nne zinazofanywa na binadamu zinazosababisha uharibifu wa mazingira.
(b) Taja majira au misimu minne ya mwaka.
8. (a) Taja faida mbili za huduma ya kwanza.
(b) Bainisha vitendo vinne utakavyozingatia kumhudumia mtu aliyezirai.
9. Orodhesha misingi minne ya kuzingatia unapofundisha vitendo vya kujifunza somo la Sayansi kwa wanafunzi wa elimu ya awali.
10. (a) Eleza kwa ufupi sababu nne zinazowafanya walimu kukwepa kufundisha somo la Vitendo vya Kujifunza Sayansi katika shule za msingi.
(b) Taja mambo manne yanayofanya mazingira ya kujifunza kuwa rafiki.

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu hii.

11. (a) Fafanua mambo matano yanayodhihirisha umuhimu wa utafiti wa kielimu.
(b) Eleza mambo manne ya kuzingatia unapotaka kupata taarifa za mtoto anayesoma elimu ya awali katika shule ya msingi.

- (c) Jadili mambo manne muhimu ya kuzingatia wakati unapofanya utafiti kwa kutumia somu ya maswali dodoso na mwongozo wa usaili.
12. (a) Bainisha mambo manne yanayoonesha umuhimu wa chakula katika mwili wa binadamu.
- (b) Je, ni madhara gani yanayomkabili mtoto kutokana na ukosefu wa lishe bora? Jadili madhara manne.
- (c) Eleza madhara manne yanayotokea kama chakula hakikuandaliwa ipasavyo.
13. (a) Kwa nini ni muhimu kutoa huduma ya kwanza kwa mtu aliyepata ajali?
- (b) Fafanua sababu tano ambazo huwa ni vyanzo vya ajali za barabarani zinazotokea mara kwa mara.
- (c) Jadili vyanzo vitano vya majanga ya asili.
- SEHEMU C (Alama 30)**
- Jibu maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu hii.
14. Jadili namna mwalimu wa somo la Kujifunza Vitendo vya Sayansi atakavyofundisha wanafunzi wa elimu ya awali kwa kutumia njia zifuatazo:
- (a) Njia ya maswali na majibu.
- (b) Njia ya simulizi.
- (c) Njia ya michezo.
15. (a) Eleza maana ya dhana ya ujuzi katika elimu.
- (b) Fafanua maana ya ufundishaji unaozingatia ujenzi wa ujuzi.
- (c) Tofautisha upimaji wa awali, upimaji endelevu, upimaji tatuji na upimaji tamati.
16. (a) Jadili tofauti iliyopo kati ya ujenzi wa dhana na ujenzi wa maana.
- (b) Eleza changamoto tano zinazokabili ufundishaji katika darasa la elimu ya awali nchini Tanzania.
- (c) Bainisha nyanja za upimaji wa kielimu na ngazi zake.